

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA A**

**682**

**VITENDO VYA KUJIFUNZA HISABATI**

**Muda: Saa 3**

**Jumatano, 06 Mei 2015 asubuhi**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama 40, sehemu B na C zina alama 30 kila moja.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. **Andika Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Bainisha hatua nne za kuzingatia wakati wa kufundisha kusoma namba 1 hadi 5 kwa watoto wa elimu ya awali.
2. Chora maumbo manne ambayo watoto wa elimu ya awali hujifunza/hufundishwa.
3. Fafanua ujuzi unaotarajiwa kujengwa kwa mtoto wa elimu ya awali baada ya kujifunza matendo ya kihisabati.
4. Elezea kwa kifupi jinsi utakavyowajengea watoto wa elimu ya awali dhana ya vipimo ili kutofautisha kati ya kipimo kimoja na kingine.
5. Orodhesha mbinu nne anazoweza kutumia mwalimu katika kufundisha mada ya matumizi ya fedha.
6. Andika mbinu nne anazoweza kutumia mwalimu katika kufundisha mada ya majira ya siku.
7. Eleza kwa kifupi hatua nne za kuzingatia wakati wa kufundisha mtoto kuhesabu vitu halisi hadi 5.
8. Orodhesha mbinu mbili anazoweza kutumia mwalimu katika kufundishia mada ya urefu kwa ufanisi.
9. Fafanua kwa kifupi unavyoweza kutumia kadi za namba katika kufundisha kusoma namba 1 hadi 5.
10. Eleza kwa kifupi namna unavyoweza kufundisha thamani kubwa na thamani ndogo ya fedha za Tanzania.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii.

11. Fafanua maumbo ya namba 1 hadi 9 ambayo hutumika katika kufundisha kusoma namba kwa watoto wa elimu ya awali.

12. Eleza umuhimu wa michezo mbalimbali katika ufundishaji wa vitendo vya kujifunza hisabati.
13. Kwa kutumia michoro, oneshwa zana mbili zinazotumika katika kufundisha/kujifunza namna ya kujumlisha namba kwa watoto wa elimu ya awali.

### SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii.

14. Eleza umuhimu wa kufanya uchambuzi katika muhtasari wa vitendo vya kujifunza hisabati kwa shule za elimu ya awali.
15. Bainisha matumizi ya fedha ya kitanzania ambayo watoto wa elimu ya awali hujifunza/hufundishwa.
16. (a) Eleza ni kwa nini wakati wa kuhesabu namba ni muhimu mwalimu awe na vihesabio.  
(b) Bainisha vitendo vitatu anavyopaswa kuvifanya/kufundishwa mtoto wa elimu ya awali ili kujenga dhana ya namba.